# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
# BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO
## Songea VTC
## 2024

Simu: 02502602442
P. O. Box 902
Songea,

Nukushi: 02502602410
songeavtc@veta.go.tz
www.veta.go.tz

Kumb. Na;
11/12/2023

Ndugu

______________________________

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUO CHA

Songea VTC Mwaka 2024

MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika

   Fani ya _________________________

   Katika ngazi ______________

   mwaka wa I Day

2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka miwili - mitatu (2-3)
3. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe 15/01/2024
4. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa
5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa
6. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua
7. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo
8. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako chuoni
9. Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyoambatanishwa na barua hii
10. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Lipa mapema ili uweze kusajiliwa. Fedha ikishalipwa hairudishwi. Kama fedha za tahadhali (caution Money) hazikutumika zitarudishwa
11. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua chuo

____________________________

Eliya Ndiwu

MKUU WA CHUO

SONGEA VOCATIONAL TRAINING CENTRE (VETA) VTC PRINCIPAL P.O.BOX 902 SONGEA

## MAHITAJI MUHIMU KWA MWANAFUNZI KWA MWAKA WA MAFUNZO 2024

**MAELEKEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/ MLEZI / MDHAMINI NA MWANAFUNZI**

1. Unatakiwa uwe na vifaa vifuatavyo kwa matumizi yako chuoni.

***1.1*** Mashati mawili (2) meupe (mikono mifupi) ya "Tetron". ***KWA WAVULANA TU***

1.2 Jozi moja ya viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi (safety boot) → kwa fani za ujenzi,useremala,umeme,umeme wa magari,ufundi magari, ufundi bomba na uungaji vyuma.



1.3 Jozi moja ya viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi kwa fani za ushonaji na uhazili. →



1.4 Vifaa vya somo la Hesabu na Uchoraji (Mathematical set).

1.5. Unatakiwa uwe na **karatasi nyeupe (Photocopy paper) A4** aina ya ***'Mond No. 1'*** - "ream" moja

**1.6.** Unatakiwa uwe na **Sweta rangi ya Blue**

1.7 Unatakiwa kuvaa **soksi nyeupe/nyeusi** wakati wote uwapo chuoni.

1.8. Unatakiwa uje na **fyekeo (slasher).** ***KWA FANI ZA MVM, PPF, DSCT NA MB.***

***1.9*** Unatakiwa uje na jembe na mpini. ***KWA FANI ZA SCA NA WF.***

***1.10*** Unatakiwa uje na **fagio (chelewa)**. ***KWA FANI ZA EL, CJ NA AE.***

1.11 Unatakiwa uje na madaftari 6 (2quire) na daftari moja la somo la michoro (Technical drawing)

***1.12*** **Unatakiwa uje na namba ya NIDA kwa waliotimiza miaka 18. *(NI LAZIMA).***

2. Jedwali lifuatalo linaonyesha mchanganuo wa malipo ya ada na michango mingine

**MUHULA WA I**

| Na. | HITAJI | NGAZI YA KWANZA (LEVEL ONE) (Tshs) | NGAZI YA PILI (LEVEL TWO) (Tshs) | NGAZI YA TATU (LEVEL THREE) (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ada | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| 2. | Tahadhari | 5,000 | - | 5,000 |
| 3. | Michezo | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 4. | Kitambulisho cha Mwanafunzi | 5,000 | - | 5,000 |
| 5. | Nembo za VETA | 5,000 | - | 5,000 |
| 6. | Suruali za chuo (2) | 44,000 | - | 22,000 |
| 7. | Overall/Overcoat | 32,000 | - | 32,000 |
| 8. | Fulana/TShirt (2) | 30,000 | - | 15,000 |
| 9. | Blouse (2)- ***kwa wasichana tu*** | 30,000 | - | 15,000 |
| 10. | Bima Ya Afya **(Kwa wasio na Bima ya Afya)** | 50,400 | 50,400 | 50,400 |
| **Jumla (Tsh.)** | | **Wasichana: 241,400**<br>**Wavulana: 211,400** | **90,400** | **Wasichana:189,400**<br>**Wavulana: 174,400** |

**Ukifika kwa mhasibu wa chuo utapewa control number zifuatazo kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza:**

i. **30,000 – Ada – kwa wote**
ii. **161,000 – Michango mingine – kwa wasichana tu**
iii. **131,000 – Michango mingine –kwa wavulana tu**
iv. **50,400 – Bima ya afya –kwa wote (Kwa wasio na Bima ya Afya)**

**MUHULA WA II**

| Na. | HITAJI | NGAZI YA KWANZA (LEVEL ONE) (Tshs) | NGAZI YA PILI (LEVEL TWO) (Tshs) | NGAZI YA TATU (LEVEL THREE) (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ada | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| 2. | Ada Ya Mtihani | 25,000 | 30,000 | 35,000 |
| 3. | Mahafali | 15,000 | 20,000 | 20,000 |
| **Jumla (Tsh.)** | | **70,000** | **80,000** | **85,000** |

Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu 1 na 2 kama vilivyotajwa hapo juu. Lipa mapema ili uweze kusajiliwa. Fedha ikishalipwa hairudishwi.

Wakati wa kusajiliwa unatakiwa afike na stakabadhi ya malipo ya ADA na michango mengine, **Vivuli halisi vya vyeti** na fomu ya uthibitisho wa afya yako toka kwa daktari wa Hospitali ya Serikali au Hospitali inayotambuliwa na Serikali.

**NB.** MALIPO YOTE YATAFANYIKA KWA NAMBA MAALUMU “CONTROL NUMBER” INAYOPATIKANA KWA MHASIBU CHUONI VETA SONGEA. **ISIPOKUWA FEDHA YA BIMA YA AFYA (UTAPEWA CONTROL NAMBA KUTOKA BIMA YA AFYA WAKATI WA USAJIRI)**

**Mwanafunzi aje na risiti ya Benki inayoonesha jina la mwanafunzi aliyelipiwa.**

Kwa huduma za malipo piga simu 0738 102 147 au 0755 096 880.

**KARIBU CHUO CHA VETA – SONGEA**

**Uongozi wa Chuo unakupongeza kwa hatua hii uliyofikia**

**Kwa ufafanuzi zaidi piga namba zifuatazo: 0738 102 147**

**VET FORM - 1G**

**VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY**

**TRAINEE PERSONAL RECORD FORM**

Centre ........................................ Workplace ............................

1. Personal information

Name ..........................................................................................

Age..................................... sex.......................................... (F/M)

Date of birth: date.........................Month ........................year.....................................

Place of birth: Village ........................... Ward..................................Division .................

District......................................................... Region..................................................

Religion............................................................... Telephone ....................................

Disability (mention if any)...................................................................................

Level of Education.......................................year of completion ....................................

Name of the school attended .........................................Region....................................

Work Experience...........................................................................................................

Name of Guardian..................................................relationship...................................

Contact address....................................................Telephone ....................................

2.0 Admission information

Trainee selected from..........................................................................

Registration number ..........................................................................

Date of admission..........................................................................

Certificate number ................Drop out date...................Reason..................................

VET DECL FORM -1F

## MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

a) MWANACHUO

Mimi ........................................................... ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

Sahihi................................................Tarehe..................................................

b) MDHAMINI

Mimi......................................................ambaye ni......................................wa mtajwa hapo juu nathibitisha kuwa nitamdhamini na nitamlipia gharama zote za mafunzo ikiwa ni ada na gharama nyingine kama ilivyoelekezwa katika maelezo ya kujiunga na chuo na nauli ya kwenda na kurudi nyumbani wakati wote wa likizo na baada ya mafunzo.

Sahihi..........................................Tarehe.....................................

VET MED FORM - 1E

# VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

## MEDICAL EXAMINATION FORM

Date................................

The Medical Officer

.............................................

.............................................

.............................................

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:

Name of trainee...........................................................................................................

Please examine the above named trainee to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an..........................................................................

Eyesight ........................................................................................ .

Hearing.........................................................................................................

Assma............................................................................................................

Other serious diseases..............................................................................

MEDICAL CERTIFICATE:

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above.

Date………………………………………. Designation………………………………….

Signature and official stamp…………………………………………….

# SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI WA KUTWA

**ILI KUFANIKISHA MAFUNZO YA AWALI YA UFUNDI KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO:-**

## 1. MAHUDHURIO:

(a) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya muda ulipangwa kufika chuoni (saa 1:30 asubuhi)
***Adhabu kali itatoiewa kwa wachelewaji***.

(b) Mwanafunzi hatakiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na mwalimu (Mkuu wa kitengo).

(c) Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua ni lazima habari/taarifa zifike chuoni, bila ya kufanya hivyo ni kosa.

(d) Mahudhurio chini ya **85%** mwanafunzi atanyimwa cheti cha kuhitimu.

## 2. MAVAZI:

(a) Sare ya chuo ni suruali ya blue na shati jeupe mikono mifupi. Sare hiyo ivaliwe wakati wote wanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Wakati wote shati/Tshirt liwe limechomekewa na nje ivaliwe sweta ya blue.

(b) Overoli livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu

(c) Viatu vyenye visigino virefu na kandambili au viatu vya wazi (sandals) **Haviruhusiwi** kuvaliwaa chuoni.

## 3. USAFI WA MWILI:

(a) Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili, mkufu na mapambo ya aina yoyote ile kama kuchora mwili kwa kipindi chote cha mafunzo.

**(b) Nywele kwa wavulana**
(i) Zikatwe ziwe fupi sana, KIPARA hairuhusiwi kabisa
(ii) Ndevu Mustaji, Sharafa, Sharubu aina zote haziruhusiwi

**(c) Nywele kwa wasichana**
(i) Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma (mistari isipungue 3 na isizidi 5).
(ii) Kucha zisifugwe kabisa wala kupakwa rangi.

4. **WIZI WA AINA YOYOTE:**

Vitedo vyovyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au ya mwanafunzi mwenzake, hatua kali za kisheria zitachukuliwa mara moja ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo na kumkabidhi polisi.

5. **UPOTEVU:**

(a) Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa na ukakinunue kifaa chenyewe au ulete badala ya ulichokipoteza.
(b) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo bila kibali maalumu.
(c) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.

6. **UGOMVI:**

Ugomvi, kupigana na kushambuliana ni makosa ya jinai atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kukabidhiwa polisi.

7. **ULEVI:**

Iwapo itabainika Mwanafunzi analewa, au kuonekana katika sehemu za kileo, anavuta bangi au madawa ya kulevua adhabu yake ni kuachishwa masomo.

8. **MAPENZI:**

Uhusiano wa kimapenzi kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi/mwalimu na mwanafuzi hauruhusiwi kabisa.

9. **MIGOMO:**

Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. atakayeshawishi au kusababisha migomo hatua kali za kisheria zitachukuliwa mara moja.

10. **LUGHA:**

Lugha inayotumika kuendesha masomo ni kiswahili na kiingereza.

11. **JINA:**

Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho na ajulishwe Mkuu wa chuo mara moja.

12. **SIMU ZA MKONONI:**

Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi katika mazingira/eneo la chuo. Iwapo utakutwa na simu katika mazingira/eneo la chuo, simu yako itachukuliwa na kupasuliwa mbele yako.